

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: 026-2322129
Nukushi: 026 -2322126
Baruaapepe: km@michezo.go.tz
Tovuti: www.michezo.go.tz



Mji wa Serikali- Mtumba,
Mtaa wa Michezo,
S. L. P 25,
40481 DODOMA.

Dar es Salaam
25 Oktoba, 2023

TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU KUVUJA MAJI KATIKA UWANJA WA BENJAMIN MKAPA

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imeona picha jongefu (video clip) inayoendelea kusambaa kwenye mitandao ya kijamii ikioneshaa kuvuja maji katika moja ya sehemu ya Uwanja wa Benjamin Mkapa ulipo jijini Dar es salaam.

Wizara inapenda kuujulisha umma kuwa tukio hilo linatokana na ukarabati mkubwa unaoendelea katika uwanja huo ambao mpaka sasa umefikia asilimia 11 na unatarajiwaa kukamilika mwezi Agosti, 2024 kulingana na mkataba wa Mkandarasi.

Hata hivyo kutokana na uhitaji mkubwa wa kufanyika kwa Mechi za Ligi ya Mpira wa Miguu Afrika (AFL) na mechi chache za Ligi Kuu ya Mpira wa Miguu Tanzania Bara imeilazimu Wizara iruhusu uwanja wa Benjamin Mkapa utumike wakati baadhi ya kazi zikiwa zinaendelea zikiwemo za ukarabati wa mifumo ya maji, umeme, viyoyozi na viti.

Wizara inawasihi wananchi na wadau wa michezo kupuuza upotoshaji unaoendelea kufanywa na baadhi ya watu kuhusu hali ya uwanja huo na kuleta tataruki isiyo ya lazima.

Aidha, tunatoa wito kwa wananchi na wadau wote wa mpira wa miguu kuwa wavumilivu kwa mapungufu yatakayojiteza pale itakapolazimu Uwanja wa Benjamin Mkapa kutumika kwa mechi wakati ukarabati ukiwa unaendelea.

Imetolewa na:-

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Aron Msigwa'.

Aron Msigwa

MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI